TANGAZO LA SERIKALI NA. 142 la tarehe 3/3/1023

SHERIA YA MIPANGO MIJI,

(SURA YA 355)

# AMRI

*(Imetolewa chini ya kifungu cha 8(1) na 23(1))*

AMRI YA MIPANGO MIJI YA KURASIMISHA MAKAZI YASIYOPANGWA KATIKA ENEO LA MADIZINI, ILULA SOKONI, ILULA MWAYA, MTUA, NGELANGO, MATALAWE, IGUNGA, ITUNDA, DINGINAYO, ITABALI, IKUVALA, MASUKANZI, IKOKOTO YA MWAKA, 2023

Jina

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Mipango Miji ya Kurasimisha Makazi yasiyopangwa Eneo la Madizini, Ilula Sokoni, Ilula Mwaya, Mtua, Ngelango, Matalawe, Igunga, Itunda, Dinginayo, Itabali, Ikuvala, Masukanzi, Ikokoto ya Mwaka, 2023.

Utangazaji wa eneo la upangaji Sura ya 355

2. Eneo lililobainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa eneo la upangaji (mpango wa urasimishaji) kwa madhumuni ya Sheria ya Mipango Miji.

Mpango katika eneo la kwenye Jedwali

3. Mipango ya jumla na kina katika eneo la kwenye Jedwali itaandaliwa na kuhifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Mipango Miji na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kilolo.

———

JEDWALI

———

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

Eneo la upangaji lipo ndani ya mipaka ifuatayo:-

“Unaanzia kwenye barabara kuu ya Iringa – Kising’a kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba HIA 265 yenye majira – nukta 813320. 4395MS, 9114959.7549KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Mashariki katika uelekeo wa uelekeo wa $55^0$ 36’ 38’’ kwa kufuata mto Mtitu kwa umbali wa kilomita 0.44 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba HIA 291 yenye majira –nukta 814245.4241MS, 9115592.8555KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini katika uelekeo wa $168^0$ 45’ 53’’ kwa umbali wa kilomita 2.5 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba HIA 267 yenye majira – nukta 814948.5633MS, 9112053.1541KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Magharibi kwa kufuata mto Mtitu kwa umbali wa kilomita 1.8 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba HIA 282 yenye majira – nukta 810090.9365MS, 9112641.8017KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini kwa kufuta mto Mtitu katika uelekeo wa $14^0$ 43’ 58’’ kwa umbali wa kilomita 0.6 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba HIA 264 yenye majira – nukta 810344.8124MS, 9114665.3932KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Magharibi katika uelekeo wa $84^0$ 21’ 2’’ hadi ulipoanzia’’

Dodoma,
6 Februari, 2023

ANGELINE S. MABULA,
*Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi*